Usia

Harmonize

Watoto wangu nyie mimi baba yenu
Nina nguvu sana za kuua hata simba
Simba na makali yote
Akimuona tembo anachimba
Ila hainivimbishi kichwa

Nachapa kazi siendekezi majungu
Ridhiki anayegawa ni Mungu
Eti niende kwa mganga piga nyungu
Nimroge fulani awe pungua

Mungu akikupa kilema lazima atakupa na mwendo
Lipiza mabaya kwa wema kula maisha bila upendo

Kumdharau usiyemjua ni dhambi, dhambi
Mtangulize Mungu na dua popote kambi, kambi

Yeah this life is a gamble
Basi jitahidi kuwa humble
Usimdharau mama wa kambo
Huenda alisha kusifu kitambo

Ni usia (Huu ni usia, usia wa tembo)
Hii dunia tunapita (Huu ni usia, usia wa tembo)
Usiendekeze vita (Huu ni usia, usia wa tembo)
Usijione special special (Huu ni usia, usia wa tembo)
Ju hauijui kesho kesho kesho

Ukikosa elimu bora sio mwisho wa maisha yako
Na kuishi chini ya dola
Wala hailkuwa matakwa yako
Cha mtu ni mavi
Achana nacho tafuta chako hata kichelewe
Uwe na meza ama jamvi ridhika na ulichonacho
Omba kwa Mungu upewe

Kingi, usijione queen ama kingi
Nakujisifu akili nyingi
Kisa unamiliki shilingi, shilingi
Mmmh punguza idadi ya maadui
Maana atakaye kuzika humjui
Mwambieni huyo kaka anajiita chui
Aache kudandia bifu chanzo hukijui

Kumdharau usiyemjua ni dhambi, dhambi
Mtangulize Mungu na dua popote kambi, kambi

Yeah this life is a gamble
Basi jitahidi kuwa humble
Usimdharau mama wa kambo
Huenda alisha kusifu kitambo

Ni usia (Huu ni usia, usia wa tembo)
Hii dunia tunapita (Huu ni usia, usia wa tembo)
Usiendekeze vita (Huu ni usia, usia wa tembo)
Hakuna haja kuduniashiana misuli (Huu ni usia, usia wa tembo)
Dunia hakuna anayeijua vizuri

Zaidi ya Mungu baba, Mungu baba baba
Usia wa Tembo, Konde boy

Sponzor: www.srovnavac.cz - vyberte si pojištění online!